

1. Chombo cha Taifa letu,  
Si sawa na vya wenzetu.  
Vyao vyataka Rubani,  
Aushike usukani,  
Awe na mabaharia  
Wanaomsaidia.
2. Na kiwe kina mafuta  
Ya kutosha kukivuta  
Au kiwe na makaa,  
Kwani pia yanafaa.  
Chombo kimekamilika  
Bahari kitavuka.
3. Mamia kingapakia  
Hao huwa abiria,  
Wakisha lipa nauli  
Na bei ya maakuli  
Hawadaiwi zaidi,  
Safari kuifaidi.
4. Wanaweza wakakaa  
Sawa sawa na bidhaa,  
Wakabebwa wasibebe  
~~Libebavyo maji debe,~~ *Kama maji mwenye debe,*  
Madhali wamo kazini  
Wanamaji na Rubani —
5. Wote wanayo hakika  
Chombo chao kitavuka.  
Chombo cha Taifa letu  
Ni chombo cha kila mtu.  
Ni chombo cha makasia  
Hakibebi abiria.
6. Ni kweli kina Rubani  
Ashikaye usukani,  
Akiepushaye myamba  
Na nyangumi au mamba,  
Bali kila abiria  
Kwa kweli ni baharia.
7. Kila aliye chomboni,  
Baharia na Rubani,  
Ni mvuta makasia  
Na mhimizaji pia.  
Kwa shibe au kwa njaa  
Wanaishi kijamaa.
8. ~~Wali~~ <sup>Walo'</sup> nacho hupeana  
Wala hawana hiana,  
Waszo' nacho hawanacho,  
Si watu wenye kijicho;  
Ni waombi wa Manani  
Ahueni iwe pwani.
9. Si chombo chenye nafasi  
Kwa watu wataanasi,  
Wadai kuhudumiwa  
Wagomvi wakidaiwa;  
Siyo cha wapita njia  
Au wabaya wa nia.

10. Si chombo cha wadoezi  
Wala si chombo cha wezi;  
Si chombo chenye nafasi  
Kwa wgomvi na waasi,  
Watu wazua fitina,  
Au wadhabidhabina.

Hakina nafasi hata  
Kwa watu wenye matata;  
Kila mtu baharia  
Avuta lake kasia,  
Agombane baharini,  
Lake atavuta nani?

1962.